LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# MASHAURI YA MADAI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# MASHAURI YA MADAI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**1. MAANA YA MASHAURI YA MADAI ........ 9**
- 1.1.Anaeweza kuwa na Mgogoro ........ 9
- 1.2.Lengo la Madai ........ 9
- 1.3.Vigezo vya Madai ........ 10
- 1.4.Muda wa Ukomo wa Kupeleka Mashauri ya Madai Mahakamani ........ 10

**2. MAANDALIZI YA KUFUNGUA MADAI ........ 12**
- 2.1.Uwezo/Mamlaka ya Mahakama ........ 12

**3. UFUNGUZI WA SHAURI MAHAKAMANI ........ 13**
- 3.1.Hati ya madai inapaswa kuwa na Mambo Muhimu Yafuatayo: ........ 14
- 3.2.Kufungua Shauri Mahakamani ........ 15
- 3.3.Namna ya Kupeleka Hati ya Kuitwa Mdaiwa Shaurini (Samansi) ........ 16
- 3.4.Wajibu wa Mdaiwa baada ya Kupata Hati ya Mdai ........ 17
- 3.5.Mambo ya Kuzingatia Unapojibu Hati ya Madai ........ 17

**4. SHAURI MAHAKAMANI ........ 18**
- 4.1.Mambo Muhimu ya Kuzingatia wakati wa Kuhudhuria Mahakamani 18
- 4.2.Athari za Kutokuhudhuria Mahakamani ........ 19
- 4.3.Kurejesha Shauri Lililofutwa ........ 19
- 4.4.Wakati wa Kusikilizwa Shauri Mahakamani ........ 21

**5. UAMUZI/HUKUMU ........ 22**

**6. BAADA YA HUKUMU ........ 23**
- 6.1.Haki za Upande Usioridhika na Hukumu ........ 23
- 6.2.Rufaa ........ 24
- 6.3.Muda wa Rufaa ........ 24

**7. KUKAZA HUKUMU ........ 25**
- 7.1.Utekelezaji wa Hukumu ........ 26
- 7.2.Mahakama Inayoweza Kukaza Hukumu ........ 26
- 7.3.Njia ya Kutekeleza Hukumu ........ 27
- 7.4.Maombi ya Kutekeleza Hukumu ........ 30
- 7.5.Mali Isiyoweza Kukamatwa ........ 32
- 7.6.Kusitisha au Kupinga Utekelezaji wa Hukumu ........ 33
- 7.7.Masharti ya kuomba Kusimamisha Utekelezaji wa Hukumu ........ 33

**8. HITIMISHO ........ 34**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Ndugu Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uweo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza, kulinda na kutetea haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla; hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama wangejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo

au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu naweili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# 1. MAANA YA MASHAURI YA MADAI

Madai ni shauri kati ya pande mbili ambapo upande mmoja unadai haki dhidi ya mwingine.

### 1.1. Anaeweza kuwa na Mgogoro

Migogoro inaweza kuwa dhidi ya mtu binafsi, watu wengi, taasisi, serikali au kampuni. Upande unaofungua shauri unaitwa mdai au wadai upande unaofunguliwa shauri unaitwa mdaiwa au wadaiwa. Mashauri ya madai pia hujulikana kama Daawa, hivyo pande zinazokinzana katika daawa huitwa Wadaawa. Ikiwa ni hatua ya rufani, mlalamikaji huitwa mrufani na mlalamikiwa huitwa mjibu rufani.

### 1.2. Lengo la Madai

Upande uliopeleka shauri Mahakamani lengo lake ni kutangazwa kupata haki inayogombaniwa. Hata hivyo Mahakama kutokana na ushahidi itakaopokea inaweza kuamua kati ya pande mbili zenye mgogoro ni nani mwenye haki na pengine mdaiwa kupata haki badala ya mdai.

## 1.3. Vigezo vya Madai

i. Lazima kuwe na mgogoro baina ya pande mbili husika;

ii. Lazima kuwepo na dai la mdaiwa amekiuka haki ya mdai;

iii. Lazima madai hayo yawe halali mbele ya sheria;

iv. Madai yote yana muda maalumu wa kupelekwa Mahakamani kisheria kutegemea aina ya madai/daawa;

v. Lazima anayeyapeleka madai awe ndiye mhusika au mwakilishi wake.

## 1.4. Muda wa Ukomo wa Kupeleka Mashauri ya Madai Mahakamani

| Aina ya dai | Muda |
|---|---|
| Mikataba | Miaka 6 |
| Madhara: Kuumizwa kwa aina mbalimbali | Miaka 3 |
| Masuala ya Ardhi | Miaka 12 |
| Mashauri ya Ajira/Kazi | Siku 30 |

| | |
|---|---|
| Madai yanayohusiana na mali zisizohamishika kama ardhi na nyumba zilizoachwa na marehemu | Miaka 12 |
| Sauri la kukaza tuzo/hukumu iliyotolewa kwenye shauri la madi mfano baraza la usuluhishi | Miaka 12 |
| Sahuri linalotokana na ukiukwaji wa amri au hukumu iliyotolewa na Mahakama | Miaka 12 |
| Shauri la kugomboa mali zilizowekwa dhamana kwa mfano kuweka dhamana/ rehani nyumba au shamba ili kupata mkopo benki | Miaka 12 |
| Shauri la kudai malimbikizo ya kodi ya nyumba. | Miaka 6 |

**MUHIMU:**

Kwa maelezo zaidi, rejea kijarida cha ukomo wa muda.

Iwapo itathibitika kwamba mojawapo ya mambo muhimu yaliyoelezwa hapo juu hayakuzingatiwa na mdai, na mdai akapeleka shauri Mahakamani, shauri hilo linaweza kutupiliwa mbali/kufutwa na mdai kuwajibika kulipa gharama za upande unaodaiwa.

# 2. MAANDALIZI YA KUFUNGUA MADAI

## 2.1. Uwezo/Mamlaka ya Mahakama

Ufunguzi wa mashauri unategemea/utazingatia uwezo na mamlaka ya kisheria ya Mahakama husika kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Eneo ulipotokea mgogoro au tukio au sehemu anakoishi mdaiwa;

ii. Shauri hufunguliwa katika Mahakama iliyo karibu yenye uwezo kisheria kusikiliza hilo shauri. Mfano, Mahakama ya Wilaya ina uwezo wa kusikiliza mashauri yote yaliyotokea kwenye hiyo Wilaya ambayo ina uwezo nayo kisheria;

iii. Kiwango au thamani ya madai: mfano Mahakama ya Mwanzo ina uwezo wa kusikiliza shauri lenye thamani ya hadi milioni thelathini (30,000,000/=) kwa mali zinazohamishika kama magari na shilingi milioni hamsini (50,000,000/=) kwa mali zisizohamishika. Mahakama za Wilaya na Mkoa za (Hakimu Mkazi) zina uwezo wa kusikiliza mashauri ya thamani ya hadi

shilingi milioni mia mbili (200,000,000/=) kwa mali zinazohamishika na shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa mali zisizohamishika;

iv. Uwezo wa Mahakama kisheria kusikiliza mashauri maalumu katika sheria maalumu:- Mfano Mahakama ya mwanzo ina uwezo wa kusikiliza mashauri yote yanayohusu sheria za kimila, Kiislamu; na Mahakama Kuu ina uwezo wa kusikiliza mashauri yote ya uchaguzi na mashauri ya kikatiba.

## 3. UFUNGUZI WA SHAURI MAHAKAMANI

Ufunguzi wa shauri utategemea na Mahakama ipi shauri linafunguliwa. Kila shauri lina namna yake ya kufungua. Mfano: Mahakama ya Mwanzo, mdai anaweza kufungua kwa kufika mwenyewe Mahakamani na kueleza shida yake au kwa barua. Kwenye Mahakama nyingine kama vile Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu, mashauri hufunguliwa kwa njia ya kuandaa hati ya madai.

**3.1. Hati ya madai inapaswa kuwa na Mambo Muhimu Yafuatayo:**

a. Jina la Mahakama;

b. Namba ya shauri;

c. Majina ya Wadaawa (mdai na mdaiwa);

d. Kama mdai anamwakilisha mtu ambaye aidha hana uwezo wa kusimama Mahakamani au amepewa nguvu za kisheria lazima ioneshwe kwenye hati hiyo;

e. Anwani za mdai na mdaiwa;

f. Maelezo ya kuhusu madai na mahali, muda na wakati yalipotokea;

g. Maombi au tuzo ambayo mdai anaomba Mahakama impatie;

h. Uwezo na mamlaka ya Mahakama katika shauri hilo;

i. Sahihi ya mdai mwenyewe au mwakilishi wake anayetambulika kisheria mfano; mtoto mdogo chini ya miaka 18 au ambaye hawezi kusimamia kesi yake kutokana na ulemavu wa kimwili, mzazi wake au mlezi wake anaweza kuweka saini;

j. Kuthibitisha kwamba madai/maelezo aliyosema ni ya kweli au taarifa alizozipata anaziamini kwamba ni za kweli na aonyeshe ni zipi anazielewa mwenyewe na zipi anazopewa taarifa;

k. Kuonyesha tarehe na mahali ambapo madai hayo yanatayarishwa;

l. Mhusika aambatanishe vielelezo vya maandishi ambayo anategemea kuvitumia kuthibitisha madai yake.

## 3.2. Kufungua Shauri Mahakamani

a. Mdai anatakiwa kuandaa hati moja ya madai na kutoa nakala zisizopungua tatu lakini zinaweza kuwa zaidi ya hizo kulingana na idadi ya wadaiwa. Baada ya kuandaa hati hizo kama ilivyoelezwa hapo juu, mdai anatakiwa kupeleka hati za madai masijala ya kufungulia madai Mahakamani ili aweze kukadiriwa ada ya ufunguzi wa shauri.

b. Ada iliyokadiriwa lazima ilipwe kwenye ofisi ya fedha ya Mahakama na mdai lazima apewe stakabadhi ya serikali. Mdai/

mhusika akishapewa stakabadhi, shauri lake litasajiliwa na kupewa namba.

c. Shauri likishapangiwa Hakimu au Jaji, mahakama itapanga tarehe ya kutaja shauri na kutoa hati za kumuita mdaiwa au wadaiwa yaani (Samansi) ikiambatana na hati ya madai.

### 3.3. Namna ya Kupeleka Hati ya Kuitwa Mdaiwa Shaurini (Samansi)

a. Mdai anaweza kupeleka hati za madai kwa mdaiwa/wadaiwa yeye mwenyewe au kutumia wafanyakazi wa Mahakama wanaofanya kazi hiyo;

b. Kama hati zitapelekwa na wafanyakazi wa Mahakama, mdai atawajibika kulipia gharama hizo. Hati zikishafikishwa kwa mdaiwa/wadaiwa, lazima zisainiwe nao kama uthibitisho wa kupokelewa;

c. Kama mdaiwa/wadaiwa watakataa kwa makusudi kupokea hati za kuitwa Mahakamani, wafanyakazi wa Mahakama wataapa kwamba mdaiwa/wadaiwa wamekataa na kiapo hicho kitawasilishwa

Mahakamani kama ushahidi na Mahakama ina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwa upande mmoja;

d. Hivyo ni vyema kutumia wafanyakazi wa Mahakama kupeleka hati za madai na wito kwani mdaiwa/wadaiwa wanapokataa kwa makusudi kupokea hati hizo, wafanyakazi wa Mahakama wanaapa na viapo vyao vinapokelewa kama ushahidi dhidi ya mdaiwa/wadaiwa

### 3.4. Wajibu wa Mdaiwa baada ya Kupata Hati ya Mdai

a. Kufika na kuhudhuria Mahakamani tarehe ambayo shauri limepangwa;

b. Kujibu hati za madai ndani ya muda anaotakiwa kufanya hivyo.

### 3.5. Mambo ya Kuzingatia Unapojibu Hati ya Madai

a. Izingatiwe kuwa kama kuna pingamizi la awali la kisheria, upande wowote unakusidia kuliwasilisha ufanye hivyo mapema kabla ya shauri kuanza kusikilizwa.

# 4. SHAURI MAHAKAMANI

## 4.1. Mambo Muhimu ya Kuzingatia wakati wa Kuhudhuria Mahakamani

i. Lazima wahusika wafike Mahakamani kwa siku na muda uliopangwa;

ii. Kabla ya siku ya shauri ni vizuri mdaiwa au mhusika akajitahidi kujua chumba cha Mahakama ambamo shauri lake litaendeshwa. Vile vile ajue Hakimu na Karani wa Hakimu husika pamoja na utaratibu uliopangwa kuhusiana na kuendeshwa kwa shauri lake siku hiyo, kwani shauri linaweza kuendeshwa kwenye chumba cha Hakimu huyo huyo au katika Mahakama ya wazi au chumba kingine kabisa. Kwa kawaida mashauri ya madai katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya huanza saa 2:30 asubuhi na Mahakama Kuu ni saa 3:00.

## 4.2. Athari za Kutokuhudhuria Mahakamani

i. Iwapo pande zote yaani mdai na mdaiwa hawatahudhuria Mahakamani kwa siku lililopangiwa, shauri linaweza kufutwa;

ii. Iwapo mdai hakuhudhuria bila kutoa taarifa Mahakamani, shauri linaweza kufutwa ikiwa mdaiwa ataiomba Mahama isipokuwa kama mdaiwa amekubali baadhi ya madai na Mahakama inatoa hukumu kulingana na madai aliyokubali mdaiwa;

iii. Iwapo mdaiwa atashindwa kuhudhuria Mahakamani, Mahakama inaweza kumruhusu mdai kutoa maelezo athibitishe madai yake kwa upande mmoja na hapo hukumu inaweza kutolewa upande mmoja.

## 4.3. Kurejesha Shauri Lililofutwa

Endapo mdai hakuhudhuria Mahakamani na shauri lake kufutwa, kama ana sababu za msingi zilizomzuia kuhudhuria Mahakamani, anaweza kupeleka maombi ya kisheria Mahakamani yakiambatana na hati ya kiapo cha sababu hizo ili Mahakama iweze kulirudisha shauri hilo liendelee

tena kusikilizwa. Maombi hayo yanatakiwa kupelekwa ndani ya siku 30 tangu tarehe ya uamuzi wa kutupwa au kufutwa shauri hili.

Endapo mdaiwa hakuhudhuria na ana sababu za msingi zilizomzuia kuhudhuria siku ya shauri, anaweza:

a. Kama Mahakama iliruhusu mdai kusikiliwa peke yake siku ambayo imepangwa, kabla mdai hajasikilizwa mdaiwa anaweza kutoa sababu za msingi kwa kutohudhuria kwake na endapo Mahakama itakubaliana na sababu hizo, basi ataruhusiwa kuendelea na shauri na kutoa utetezi wake;

b. Iwapo Mahakama ilitoa uamuzi au hukumu ya upande mmoja, mdaiwa anatakiwa kuomba kutengua uamuzi huo kwa kupeleka maombi ambayo yataambatana na hati ya kiapo na sababu za msingi ndani ya siku 21, na kama Mahakama itaridhika na sababu hizo, itatengua uamuzi huo na kumruhusu mdaiwa kutoa utetezi wake. Ikumbukwe kwamba, upande ulioathirika unatakiwa kuomba kutengua uamuzi huo

kama tulivyoeleza hapo juu na si kukata rufaa dhidi ya maamuzi hayo;

c. Mhusika anaweza tu kukata rufaa iwapo ataomba kutengua maamuzi hayo dhidi yake na kama atakataliwa basi anaweza kukata rufaa dhidi ya amri ya kukataliwa;

d. Ni muhimu izingatiwe kwamba, mdaiwa anapopewa ruhusu ya kuwasilisha madai yake upande mmoja haina maana kwamba lazima ashinde, anaweza kushindwa pia, na iwapo atashindwa anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi au hukumu hiyo.

## 4.4. Wakati wa Kusikilizwa Shauri Mahakamani

Jukumu la kuthibitisha madai ni la mdai mwenyewe kwa kuthibitisha madai yake kwa;

i. Kuandaa mashahidi na yeye kutoa ushahidi wake. Mashahidi hao wanatakiwa kumuunga mkono kwa kuthibitisha madai ya mdai. Ikumbukwe kwamba, Mahakama haihusiki na kumtafutia mdai mashahidi; ni jukumu lake kuhakikisha mashahidi wanafika Mahakamani kwa gharama zake. Mahakama inaweza tu kutoa hati za wito (samansi);

ii. Ikumbukwe kwamba, mdai na mdaiwa wanatakiwa kutoa idadi ya mashahidi na majina yao pamoja na vielelezo mapema kabla ya kusikilizwa kwa shauri. (Kwa maelezo zaidi rejea kijarida cha ushahidi);

iii. Baada ya mdai kuthibitisha madai yake mdaiwa atalazimika kufanya utetezi wake kwa taratibu zile zile ambazo mdai ametumia kuendesha shauri.

**KUMBUKA:**

Endapo mdai au mdaiwa atafanya kitendo chochote kinachohatarisha kitu au mali zinazobishaniwa, kama kuuza mali ambayo inabishaniwa, au kuuza mali ambayo ndiyo pekee itakayomwezesha mdai kupata haki yake dhidi ya mdaiwa, mdai au mdaiwa anaweza kuomba Mahakama itoe amri ya kusitisha kitendo hicho.

## 5. UAMUZI/HUKUMU

Baada ya Mahakama kusikiliza ushahidi wa pande zote itatoa hukumu ambayo itaeleza au kuelekeza

ni jinsi gani mshindi wa kesi anaweza kupata haki yake na kutaja haki zilizotolewa. Baada ya hukumu kutolewa, upande ulioshinda utaomba Mahakama amri ya Mahakama ambayo itabainisha haki au amri zilizotolewa na Mahakama kwa ajili ya kukaza hukumu (Decree). (Kwa taarifa zaidi rejea kijarida kuhusu hukumu).

Baada ya kupata amri ya Mahakama, mshinda tuzo itabidi atalazimika kujaza fomu maalumu za kuomba kukaza hukumu kwa namna ambayo mshinda tuzo atakuwa ameiomba Mahakama kufanya.

# 6. BAADA YA HUKUMU

### 6.1. Haki za Upande Usioridhika na Hukumu

Kwa kawaida upande ambao haujaridhika na maamuzi ya Mahakama unaweza kuiomba Mahakama:

i. Kukata rufaa (Appeal);

ii. Kuomba mapitio ya hukumu kwenye Mahakama hiyo (Review);

iii. Kuomba marejeo kwenye Mahakama ya juu (Revision).

### 6.2. Rufaa

Upande usioridhika na maamuzi ya Mahakama itabidi uombe nakala ya hukumu, amri ya Mahakama na mwenenendo wa shauri ndani ya muda ambao umepangwa kisheria.

Upande unaokata rufaa utawasilisha rufaa yake kwa kuorodhesha sababu za rufaa zilizomfanya usiridhike na uamuzi wa Mahakama iliyotoa uamuzi. Sababu hizo zinahitaji kuambatanishwa na nakala ya hukumu, mwenendo wa shauri na amri ya Mahakama (dikrii/tuzo) kama rufaa inatoka Mahakama Kuu kwenda Mahakama ya Rufaa. (Kwa taarifa zaidi rejea kijarida chetu kuhusu rufaa).

### 6.3. Muda wa Rufaa

Ni muhimu kuzingatia muda wa kukata rufaa kwa sababu kuna tofauti za muda wa kukata rufaa kufuatana na aina ya shauri na Mahakama rufaa inakopelekwa.

a. Kukata rufaa kutoka Mahakama ya Mwanzo kwenda Mahakama ya Wilaya ni siku 30 isipokuwa kwenye mashauri ya ndoa ni siku 45.

b. Kukata rufaa kutoka Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Hakimu Mkazi kwenda Mahakama Kuu ni siku 30 isipokuwa kwenye mashauri ya ndoa ni siku 45.

Endapo mrufaniwa anataka kukaza hukumu, mrufani anaweza kuomba Mahakama iliyotoa hukumu au Mahakama itakayosikiliza rufaa kusitisha kukaza hukumu hadi rufaa itakapoamuliwa.

## 7. KUKAZA HUKUMU

Kwa kawaida mara baada ya shauri kumalizika Mahakamani na mdai kushinda au kushindwa, amri ya utekelezaji wa hukumu hutolewa ili kumpa haki mshindi. Amri hii hutolewa na Mahakama baada ya kutafsiri barabara maelezo ya hukumu ili kuainisha amri ya utekelezaji wa hukumu. Mara nyingi mshindi hukaa nyumbani akingojea mshindwa atekeleze hukumu kwa hiari yake mweneywe. Si mara nyingi jambo kama hilo kutokea. Hivyo ni nia ya kijitabu hiki kukuelezea utaratibu unaotakiwa kufuata ili kutekeleza hukumu.

## 7.1. Utekelezaji wa Hukumu

Hii ni njia ambayo mtu aliyepata haki au ushindi Mahakamani anaweza kufuata ili kumlazimisha aliyeshindwa kutekeleza amri ya Mahakama inayoainisha haki za mshindi katika kesi. Hii inamaanisha kwamba, kushinda shauri peke yake hakumpi mtu aliyeshinda shauri hilo haki ya moja kwa moja dhidi ya aliyeshindwa, ila ni kwa njia ya kutekeleza hukumu tu mshindi katika shauri anaweza kupata haki yake.

## 7.2. Mahakama Inayoweza Kukaza Hukumu

Hukumu iliyopitishwa na Mahakama inaweza kutekelezwa aidha na Mahakama hiyo hiyo au na Mahakama nyingine baada ya kuombwa na mshindi wa hukumu. Hiyo inatazama zaidi aina ya hukumu iliyotolewa na mahali ambapo mali ya mdaiwa ipo. Kwa mfano, kama hukumu imetolewa na Mahakama ya Wilaya ya Morogoro ikimpa mdai haki ya fidia, itabidi mdai aieleze Mahakama mali za mdaiwa zilipo. Kama mdaiwa anamiliki gari lililoko Dodoma, basi mdai ataiomba Mahakama iliyotoa hukumu itoe amri ya kukamatwa kwa gari hilo huko Dodoma.

Amri hiyo ya kukamata gari itapelekwa katika Mahakama ya wilaya ya Dodoma ili Mahakama hiyo isimamie utekelezaji wa hukumu hiyo.

### 7.3. Njia ya Kutekeleza Hukumu

Kuna njia tofauti za kutekeleza hukumu. Mara nyingi inategemea aina na asili ya hukumu iliyotolewa. Baadhi ya njia hizo ni:

i. Malipo ya fedha;
ii. Kukamata mali;
iii. Kifungo cha kiraia;
iv. Akaunti ya Benki kukamatwa;
v. Kurudisha mali au kuachia mali;
vi. Mauzo ya mali.

Hizi ni baadhi ya njia ambazo mtu ambaye ameshinda hukumu anaweza kutekeleza hukumu ya Mahakama. Ufuatao ni ufafanuzi wa njia zilizotajwa hapo juu.

a. Malipo ya fedha

Malipo yanaweza kufanyika aidha katika Mahakama ambayo imetoa hukumu au moja kwa moja kwa mtu ambaye ameshinda

hukumu. Pia malipo yanaweza kufanyika kwa namna nyingine yoyote kama Mahakama inavyoona inafaa.

b. Kukamata Mali (Attachment of property)

Utekelezaji wa hukumu unaweza kufanyika kwa kukamata mali ya mdaiwa ili iweze kuuzwa na wakala wa Mahakama na fedha zilipwe kwa mtu aliyeshinda hukumu. Mshindi wa hukumu ni lazima ajaze fomu maalumu na aainishe ni mali gani ya mdaiwa ikamatwe ili aweze kupata haki yake baada ya mali hiyo kukamatwa na kuuzwa na dalali wa Mahakama.

c. Kifungo cha kiraia (Arrest and detention as civil prison)

Ikiwa Mahakama imetoa amri katika hukumu dhidi ya mtu au upande mmoja wa shauri ulioshindwa, basi ni lazima mtu huyo atekeleze hukumu hiyo kulingana na amri hiyo ya Mahakama. Kushindwa kufanya hivyo, Mahakama ina uwezo wa kutoa amri ya kukamatwa mtu huyo ili atumikie kifungo kama mfungwa wa kiraia mpaka hapo atakapolipa deni lake kwa mshindi wa kesi.

Ila, ikumbukwe kwamba mfungwa wa kiraia ni tofauti na wafungwa wengine kwa sababu mfungwa wa kiraia atalipiwa gharama za kukaa kifungoni na mshindi katika hukumu mpaka pale atakapokubali kutekeleza hukumu. Mfungwa wa kiraia hapaswi kutumikia adhabu au kufanya kazi za gereza anapotumikia kifungo chake. Kifungo cha kiraia si adhabu, bali ni njia ya kumshinikiza aliyeshindwa kwenye kesi atekeleze hukumu kama ilivyoamriwa na Mahakama.

d. Kukamatwa kwa Akaunti ya Benki (Garnishee Order)

Njia hii ya utekelezaji wa hukumu hutokea pale ambapo wahusika yaani mdai na mdaiwa walikuwa wakifanya mahusiano yao ya malipo kupitia benki na hivyo inakuwa rahisi kujua akaunti ya mdaiwa iko katika benki gani. Ama pale ambapo mshindi wa shauri anapokuwa na ufahamu halisi wa nambari za akaunti za mdaiwa. Pia Mahakama inaeweza kutoa amri kuwa mdaiwa amlipe mshindi wa hukumu kiasi

cha fedha anachodaiwa kupitia hundi au akaunti yake ya benki.

e. Kurudisha Mali au Kuachia Mali

Mahakama ina uwezo wa kutoa amri maalumu ya kurudisha mali au kuachia mali ambayo ilikuwa chini ya mdaiwa kabla ya hukumu kutolewa na kurudisha mali hiyo kwa mmiliki halali wa mali hiyo. Kwa mfano, mdaiwa ambaye amevamia shamba la mtu au watu, amri ya kuachia mali kwa mtu aliyevamia shamba hilo hutolewa na Mahakama.

f. Mauzo ya Mali

Hukumu iliyotolewa na Mahakama inaweza kutekelezwa kwa Mahakama kutoa amri ya uuzaji mali ya mdaiwa katika kesi hiyo. Kazi hiyo itafanywa na dalali wa Mahakama na dalali huyo kuwasilisha mapato yaliyopatikana kutokana na mauzo hayo; na Mahakama kumpatia aliyeshinda shauri haki yake anayostahili.

## 7.4. Maombi ya Kutekeleza Hukumu

Kama tulivyo ainisha hapo awali kwamba kushinda shauri la madai peke yake hakumpi aliyeshinda hukumu haki ya moja kwa moja aliyopewa na mahakama. Ni lazima mtu aliyeshinda shauri kuiomba Mahakama amri ya utekelezaji wa hukumu hiyo.

Mara nyingi maombi ya amri ya utekelezaji wa hukumu ni lazima yafanywe kwa maandishi. Hata hivyo kuna wakati mwingine maombi ya mdomo yanaweza kufanywa na Mahakama ikaamuru utekelezaji wa hukumu ufanyike. Mahakama hutoa fomu/nyaraka maalumu ya utekelezaji wa hukumu ambayo hujazwa na mwombaji. Fomu hiyo lazima iwe na mambo yafuatayo:-

a. Nambari ya ushauri;
b. Majina ya mwombaji na mdaiwa;
c. Tarehe ya amri ya Mahakama;
d. Maelezo kama rufaa imekatwa au la;
e. Kama ni ombi la mara ya kwanza au la;
f. Kiasi cha fedha na/au mali inayodaiwa;
g. Kiasi cha gharama za kuendesha shauri;
h. Jina la mtu ambaye hukumu inatekelezwa dhidi yake;

i. Aina ya utekelezaji wa hukumu. Kwa mfano malipo;kukamata mali, kuuza, n.k.

## 7.5. Mali Isiyoweza Kukamatwa

Siyo kila aina ya mali inaweza kukamatwa kwa minajili ya utekelezaji wa hukumu. Hii ni kwa sababu mali nyingine zikikamatwa zinaweza kuathiri haki ya kuishi ya mdaiwa. Mali za aina hiyo ni kama zifuatazo: -

i. Nguo za kuvaa, vyombo vya kupikia, mashuka, vitanda, sahani pamoja na vyombo vya matumizi ya nyumbani kama vile ndoo, vijiko, n.k;
ii. Zana za kazi kama vile zana za uchoraji, kama anayedaiwa ni mchoraji, zana za kilimo kama mdaiwa ni mkulima, mfano; misumeno, majembe n.k;
iii. Nyumba wanayoishi wanafamilia;
iv. Mshahara wote mzima wa mdaiwa (anaweza tu kukabidhi 1/3 ya mshahara;
v. Vitabu vya benki, na vitabu vya mahesabu;
vi. Nyumba ya mkulima;
vii. Marupurupu ya mfanyakazi.

### 7.6. Kusitisha au Kupinga Utekelezaji wa Hukumu

Ikiwa Mahakama imetoa amri ya utekelezaji wa hukumu kwa njia zilizoainishwa hapo juu, mtu ambaye hukumu itatekelezwa dhidi yake anaweza kuiomba Mahakama kusimamisha au kuondoa amri ya utekelezaji wa hukumu ilimradi awe na sababu maalumu zinazoridhisha Mahakama kuona kuwa utekelezaji wa hukumu utakiuka misingi ya haki.

### 7.7. Masharti ya kuomba Kusimamisha Utekelezaji wa Hukumu

Kwa mwombaji yeyote anayetaka kuomba kusimamisha utekelezaji wa hukumu ya Mahakama, ni lazima atekeleze masharti yafuatayo:-

a. Atafanya hivyo kwa hati maalumu kwa hakimu au jaji (chamber summons) inayoambatana na hati ya kiapo cha mwombaji. Hati hiyo inaweza kuwasilishwa katika Mahakama ambayo itatoa amri au Mahakama itakayosikiliza rufaa hiyo.

## 8. HITIMISHO

Ni dhahiri kwamba mara baada ya kutolewa hukumu, mshindi ana hiari kuomba nakala ya hukumu pamoja na nakala ya amri (Decree) ili aweze kujaza fomu/ nyaraka zinazoweza kupelekea kutolewa kwa amri ya utekelezaji wa hukumu. Kutofanya hivyo kutamnyima mshindi kupata haki yake. Hivyo basi, mshindi asikae nyumbani kusubiri mdaiwa kutekeleza hukumu bila ya kuamriwa na Mahakama kufanya hivyo.

Ndugu msomaji, tunatumaini kuwa mpaka sasa unafahamu kabisa ni nini cha kufanya ili uweze kupata haki yako baada ya Mahakama kutoa hukumu kwa kukupa wewe ushindi. Tunaomba elimu hii unayoipata uitoe kwa jamii nzima ili kila mmoja aweze kujua ni nini cha kufanya baada ya kupata hukumu iliyompa ushindi.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*